

Mwingiliano Wa Utanzu Wa Modern Taarabu- Mipasho Na Maigizo

Jackline Njeri Murimi

School of Education, Tom Mboya University College

A constituent College of Maseno University

Ikisiri

Muziki wa taarab umepata mabadiliko makubwa na kusababisha kuwepo kwa aina mbili kuu za Taarab: Taarab Asili na *Modern Taarab*. Utafiti huu ulihakiki mwingiliano tanzu katika Taarab-Mipasho. Malengo ya Makala hii yalikuwa ni kuchanganua miktadha mbalimbali ya mwingiliano tanzu katika muziki wa Taarab ya Mipasho na utanzu wa maigizo na kutathmini dhima ya mwingiliano huo katika muziki wa Taarab ya Mipasho. Makala hii iliongozwa na nadharia ya mwingilianomatini iliyoasisiwa na Julia Kristeva (1960) baada ya kuizua kutokana na nadharia ya Mikhail Bakhtin ya Usemezano ambapo imetumika kushughulikia mwingiliano tanzu katika Taarab-Mipasho. Pia nadharia hii imetumika katika kufafanulia uhuru na ubunifu wa mtunzi wa kuingiza vipengele vipya katika kazi. Utafiti huu ulichukua muundo wa kimaelezo. Ukusanyaji data ulihusisha usikilizaji, utazamaji na unukuzi daftariini wa nyimbo za Taarab ya Mipasho ili kupata mistari, vifungu vya maneno na stanza zilizobainisha mwingiliano tanzu. Sampuli ya utafiti ilikuwa nyimbo 32 za muziki wa Taarab ya Mipasho ambazo ziliteuliwa kumaksudi. Uchanganuzi na uwasilishaji wa data ulitolewa kwa njia ya maelezo ya kina yaliyohusisha udondoaji na ufafanuzi wa mistari, vifungu vya maneno na stanza zenye kudhihirisha mwingiliano tanzu kutoka kwa data asili. Kutokana na matokeo ya utafiti, mwingilianotanzu mkubwa ulibainika katika uwasilishaji wa muziki wa *Modern Taarab* ya Mipasho uliorejelewa. Utafiti huu unawachochea wahahakiki wengine wa fasihi simulizi katika kufanya uchunguzi zaidi katika mitindo mingine ya nyimbo za *modern taarab* kwa misingi ya nadharia mbalimbali za fasihi. Aidha, kutokana na utafiti huu, ilitarajiwa kuwa watafiti wataweza kulinganisha na kulinganua mitindo tofauti ya taarab. Hatimaye, mtafiti anapendekeza tafiti zaidi zifanywe ili miongoni mwa mengine, kusuluhisha mgogoro kuhusu taarab ya mipasho, uwezekano wa kujumuisha nyimbo za taarab miongoni mwa vipera vya utanzu wa nyimbo katika awamu zote za usomi na uhakiki wa fasihi simulizi kwani muziki wa taarab na hasa mipasho bado unahitaji utafiti Zaidi.

Key words: Mwingilianotanzu; Mwingilianomatini; Taarab; Modern Taarab; mipasho; maigizo

UTANGULIZI

Kwa mujibu wa Mulokozi (1996) na Muiruri (2006: 71), maigizo ni utanzu wa fasihi simulizi wenye mpangilio wa maneno ambayo huambatana na utendaji wa wasanii. Maigizo ni sanaa inayotumia watendaji kuiga tabia au matendo ya watu na viumbe wengine ili kuburudisha na kutoa ujumbe fulani. Mulokozi anasema kuwa maigizo ya Kiafrika huambatana na ngoma, mtambaji wa hadithi au matendo ya kimila. Utanzu wa maigizo umeingiliana na ule wa nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho* zilizorejelewa katika utafiti huu kwa njia tofauti hususan maleba tofauti tofauti yaliyovaliwa, matumizi ya ishara na ishara za nyuso na hali kadhalika miondoko mbalimbali ya mwili. Wasanii katika maigizo huiga mambo yanayopatikana na namna yanavyoonekana katika jamii. Maigizo kama kipengele cha sanaa ya maonyesho huwa na sifa kama vile dhana inayotendeka, jukwaa, watendaji, hadhira, muktadha wa kisanii wenye ubunifu na kusudio la kisanii. Maigizo hutumia maleba maalumu kama vizuizui. Katika maigizo, matendo yaigizwayo na wasanii huwa si halisi kwa sababu wahusika wa kifasihi huwa si watendaji halisi ila hujitwika uhusika kwa muda tu kwa kusudi la kuwasilisha ujumbe ambao ungewasilishwa na wahusika halisi katika jamii. Katika *Modern Taarabu-Mipasho*, mhusika aghalabu huigiza matini ya nyimbo zake katika uimbaji wake ili kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe.

MWINGILIANO WA UTANZU MODERN TAARABU- MIPASHO NA MAIGIZO

Katika *Modern Taarabu-Mipasho*, maigizo yamefanywa kulingana na maudhui mbalimbali kama yalivyojitokeza katika nyimbo husika (mfano umetolewa katika kiambatisho-**Mpenzi Chocolate-Mzee Yusuf**). Mhusika katika utendaji wake ameigiza wimbo huu kwa kutumia ndege aina ya helikopta kuonyesha ufalme wake wa mapenzi. Aidha, katika uigizaji huu, Mzee Yusuf anadhihirisha uigizaji wa kifilamu ambapo anapoanza kuimba anatua kutoka kwa ndege. Amejitoa katika ulimwengu wake wa utamaduni wa Mwafrika na kuingia katika ulimwengu wa uigizaji wa Kimagharibi. Usafiri kwa ndege si wa kawaida kwa watu wachochole. Usafiri wa aina hii ni wa wachache ambao wanajiweza kifedha. Hili ni dhihirisho kuwa yeye kweli kama mfalme wa mapenzi ana uwezo wa kifedha. Ameabiri helikopta tayari kuondoka ili afike na kutua uwanjani palipo na hadhira yake inayomsubiri kwa hamu kumsikiliza akiwasilisha nyimbo zake za mipasho.

Mzee Yusuf amedhihirisha mwingiliano kati ya utanzu wa filamu, maigizo na *Modern Taarabu-Mipasho* akiwa katika ndege aina ya helikopta. Uigizaji huu pia ni namna ya kuonyesha mawazo yake ya kisasa ambapo anatumia usafiri wa kisasa, hali ambayo inaambatana na aina ya nyimbo anazoimba-*Modern Taarabu-Mipasho* ambazo zimejitenga kutoka Taarabu asili yenye kufuata utendaji na uwasilishaji wa kitamaduni. Aidha, Mzee Yusuf ameigiza akiwa amealia mavazi ya kifalme au Sultan huku akihudumiwa na wafanyikazi kadhaa katika uigizaji wake ili kuonyesha utukufu na haiba inayoambatana na maisha ya kifalme. Amevaa vazi laini la sari na kuzungukwa na mapambo mbalimbali katika chumba chake. Maudhui makuu katika wimbo huu ni mapenzi motomoto anayopewa mhusika na mpenzi wake ambaye anammiminia sifa teletele. Kukiwa na joto, mpenziwe anamtuliza kwa kumpepea na kukiwa na baridi kali, mpenziwe anampa joto. Anaigiza akilakiwa na kusaidiwa kubeba mizigo mizito, hata akifuliwa nguo zake chafu na hata kupuuliziwa na kulishwa kama anavyofanyiwa mtoto kutokana na mapenzi mengi kwake.

Katika muktadha wa wimbo huu wa *Modern Taarabu-Mipasho*, mhusika amejawa na bashasha na ndipo anaamua kumpa mpenzi wake chokoleti na tende kudhihirisha mapenzi matamu anayopata. Aidha, analinganisha uzuri wa mapenzi anayopata na utamu wa chokoleti na tende. Hali hii ni dhihirisho la ufahamu wa mhusika kuhusu mambo ambayo hutendeka katika ulimwengu wa

kimapenzi. Kwa kawaida, watu wanapopendana hudhihirisha mapenzi yao kwa namna nyingi tofauti. Miongoni mwake ni kule kubusiana na kukumbatiana, kulakiana na kusaidiana katika majukumu mbalimbali kama vile kukuna nazi na hata kufua nguo.

Ukunaji nazi na ufuaji nguo ni kazi za wanawake katika utamaduni wa Waswahili. Kwa mwanamume kufanya kazi hizi basi itakuwa ni kwa hiari yake na kwa sababu zake binafsi. Hata hivyo, kufanya kazi hizi hakutaidunisha nafsi ya yule mwanamume kwani atakuwa amechagua yeye mwenyewe kufanya hivi. Mwanamke anayesaidiwa kufanya kazi hizi hufurahia na kuhisi amependwa na yule mpenzi wake. Katika muktadha wa wimbo huu, Mzee Yusuf aliamua kufanya kazi hizi kutokana na mapenzi mazuri ya kuridhisha aliyokuwa amepata kutoka kwa mpenzi wake. Mpenzi wake aliweza kumpikia chakula kitamu na kisha kumlisha. Katika muktadha wa utendaji wa Taarabu hii, Mzee Yusuf alimuuliza mpenzi wake ataje lolote alilotaka kufanyiwa naye angefanya ndipo mpenzi wake akaamuuliza amsaidie kukuna nazi. Kisha, Mhusika huyu anaigiza akimsaidia mkewe kufua nguo kama njia nyingine ya kuonyesha penzi lake kwake. Mwanamume wa Kiafrika akionekana akifanya kazi kama hii ya kukuna nazi, baadhi ya watu humwona kama ambaye ametawaliwa na mkewe ambapo husemwa kuwa 'amekaliwa na mkewe'.

Aidha, wapenzi huweza kutumia majina ya kuvutia na ya kilakabu kwa wapenzi wao katika kujaribu kuelezea hisia zao za kimapenzi. Sababu ni kuwa ni muhali kuweza kuzielezea hisia za kimapenzi kwa kutumia maneno ya moja kwa moja. Badala yake, maneno yenye kuleta athari za mguso na hisia za kimapenzi hutumika. Mfano: **-6-*'Yeye ndiye Chocolate wangu'***. *Chocolate* ni kitafunio ambacho huwa na sukari na kakau na ambacho huyeyuka kinapotiwa mdomoni. Ladha yake ni tamu kwelikweli na yenye harufu ya kuvutia. Aidha, anayeelezea hisia zake za kimapenzi hutumia maneno yanayodhihirisha kusalitika kwake kimapenzi kama ilivyobainika katika kiambatisho kifuatacho.

10 Unaponukia udi, malaika hunisimama mie'

21 Ye ndio kila kitu kwangu, mpenzi chocolate

22 Ye ndio binti wangu sisikizi yoyote,

23 Kama ni tamu,

24 Nairamba, alivyotia,

24 Kama ni hamu,

25 Naipenda, aniswabilia

26 Ananitia nakshi, nakshi mahamumu,

27 Kumwacha sitaki, nitajidhulumu.

28 Kidonda tamu nzi ndo hufia,

29 Hapa patamu ndio maana nimetulia

30 Dhahari wazimu champari nimevua

31 Ananitia nakshi, nakshi mahamumu

Kutokana na kifungu hiki, mhusika huyu yuko radhi kupenda mpenziwe kwa namna zote zile wala hatabanduka kamwe. Haoni haja ya kusikiza maneno ya watu wengine kuhusu mapenzi yao. Heri afie pale kama nzi kidondani! Matendo na maneno katika wimbo huu yanadhihirisha kuwa mtu akishapenda ni vigumu kumgeuza nia kwa lolote lile kama anavyodhihirisha Mzee Yusuf. Mhusika huyu anaigiza ufalme wake wa kimapenzi katika himaya yake ya kidhahania. Baadaye, Mzee Yusuf anamalizia kwa kuigiza akirejea katika kupaa na kuondoka kwa ndege iliyomleta alipoanza. Katika sehemu hii, ile ishara maarufu inayoashiria mwisho wa uigizaji katika filamu, **'THE END'** inaonyeshwa na uimbaji unakamilikia pale.

Mfano mwingine wa mwingiliano tanzu wa maigizo na *Modern Taarabu-Mipasho* umo katika kiambatisho **-Full Stop -** Taarabu iliyoimbwa naye Khadija Kopa. Mhusika huyu anatoa onyo na kutaka mambo kadhaa yakome. Miongoni mwa anayopendekeza yakome ni pamoja na wafitini wanaoingilia ndoa za watu, vijana wanaoshiriki mapenzi kiholelaholela na wanawake wanaojivunia utamaduni wa kigeni. Katika uimbaji huu Khadija Kopa ameonyeshwa akinyoosha mkono wake kila anapotaja neno '*fullstop*' kama ishara ya 'kutia kikomo'. Aidha, ametumia neno '*Fullstop*' ili kusisitiza ujumbe wake wa kutaka masuala anayotaja yakomeshwe mara moja.

Katika kuwakomesha wafitini, Khadija Kopa ametumia moto unaowaka sana na kuwaonya wasiuguse wasije wakaungua. Moto huu ni ishara ya hatari iliyomo kwa watu wale wafitini wanaoingilia ndoa za watu, wanawake wanaojivunia utamaduni wa kigeni na vijana wanaoshiriki mapenzi kiholelaholela. Pia, katika wimbo huu, mmeigizwa tabia mbaya ya wanawake wanaopigania mabwana. Ili kudhihirisha msimamo wake kuhusu kudumisha mila na utamaduni wa Kiafrika, mhusika huyu na wanaoigiza naye wanavalia khanga na shanga na kubeba vibuyu. Haya ni maleba ambayo huvaliwa katika utamaduni wa Kiafrika. Pia, uchezaji wao katika wimbo huu ni wa kitamaduni kulingana na utendaji wa nyimbo katika fasihi simulizi ya Kiafrika. Hali hii imeshadidia msimamo wa Khadija Kopa wa kudumisha utamaduni na kuasi mkengeuko unaoambatana na tabia ya kigeni. Amewaongoza vijana ambao ni wachezaji wake katika kuvaa na kucheza kwa njia ya utamaduni wa Kiafrika.

Mwingiliano tanzu mwingine kati ya utanzu wa maigizo na *Modern Taarabu-Mipasho* unapatikana kwenye kiambatisho **Utalijua Jiji-** Afua Suleiman. Baadhi ya sehemu zilizoigizwa ni pale mhusika anapomsuta mwanamke mwenzake kwa kumwambia maneno yafuatayo:

- 26. *Unaningoja njiani, madhila kunifanyia*
- 27. *Usitake ushindani, hunishindi nakwambia*
- 28. *Mimi naletewa ndani, wewe watanga na njia*
- 29. *Magomeni buguruni, ndara zakukatikia.*

Uigizaji wa sehemu hii unaonyesha wanawake wawili wakipigana baada ya mmoja kumvizia mwenzake njiani. Hii ni hali ambayo hutokea hasa baina ya wanawake washindani wa mapenzi. Mwanamke ambaye amedhulumiwa kimapenzi atafanya lolote kupigania penzi hilo hata kama ni kumvizia mbishi wake vichochoroni ili amfunze adabu kwa kumchapa. Vita hivyo huwa ni vya ghafla kwa anayevamiwa. Wanawake wanaopigana hutumia viungo vyao vya mwili kama vile mikono, miguu na hata meno katika kuwaadhibu wenzao. Aghalabu, vita vya aina hii huleta aibu kubwa pale wanawake wanaopigana wanapoangushana kiholela huku wakiraruliana nguo hivyo kuonyesha uchi wao.

Mashambulizi ya aina hii pia huwa na madhara mengi kwa wapiganao kwani huacha maumivu ya mwili pale wanapokwaruzana ngozi kwa kucha zao au wanapoumana kwa meno. Aidha, hupata majeraha ya nafsi zao kutokana na uchungu waliopata pale wanapopigana. Mahusiano baina yao huweza kuharibika kabisa kutokana na uhasama wa kimapenzi. Hii ndiyo hali inayompata mwanamke wa kwanza wakati anapoviziwa na mbishi wake anayeonekana kuwa na hamaki nyingi kutokana na hali ya mateso ya kimapenzi aliyopitia. Anabururwa huku akizabwa makofi yanayofuatana kwa mfululizo.

Katika muktadha huu, Afua Suleiman anaonekana kujigamba kuwa hashindiki katika uwanja wa mapenzi. Kisha anajigamba kuwa yeye huletewa kila kitu nyumbani ambapo katika uigizaji wa kanda hii anaonekana akiletewa mavazi kama vile khanga na mwanamume husika. Anamsuta mwanamke mpinzani wake ambaye katika kanda hii anaonekana akihangaika kutafuta hadi ndara zinakatika. Ndara kukatika ni ishara ya kutembea kwa muda mrefu katika hali ya kuhangaika akitafuta riziki. Huu ni uendelezaji wa vita vya maneno baada ya mhusika kuvamiwa kwa kuviziwa njiani. Inamlazimu amsute mpinzani wake wa mapenzi kwa maneno yaliyojaa kejeli, ya kumdunisha, kumdharau na kumuumiza moyo ili amwachie mpenzi wanayebishania. Mwanamke huyu anaonekana akiwa tayari kabisa kulinda himaya yake ya kimapenzi aliyoinyakua kutoka kwa mwanamke mwenzake kwa namna yoyote ile inayowezekana hata ikiwa ni kwa meno na ukucha.

Mwanamke aliyenyang'anywa mpenzi kwa kubaki na machungu anaweza kuamua kutafuta wapenzi wengine kama alivyofanya mrejelewa katika mpasho huu. Hii ni njia moja ya kulipiza kisasi kwa mwanamume ambaye ni mpenzi wake kwa kuleta machungu kwa mwanamume pale atakapomwona na mwanamume mwingine. Pia, ni njia ya kujipatia kipato alichokosa kutokana na kutoshughulikiwa na mwanamume aliyemwacha. Pale tu anapoingia katika mtego huu, wanaume humtumia kama kiburudisho lakini baadaye wakamsema kila anapopita kutokana na tabia yake ya kuwa uasherati. Haya yamesemwa kama inavyodhihirika katika mishororo ifuatayo:

30. *Wasela wa vijiweni, nafuu wajipatia*
31. *Uroda kwa foleni, kwako wajipendelea*
32. *Wewe gumzo mjini, watu wanahadithia*
33. *Umeachika ndoani, kwa yako mbaya tabia.*
34. *Unaogea jikoni, bafuni unapikia*

Mwanamke mwigizaji haachi kumsuta mwenzake kuhusu tabia yake mbaya. Kawaida, chakula hupikiwa jikoni. Mazingira ya jikoni yanatarajiwa kuwa safi kwa ajili ya usalama wa kiafya kwa wanaotarajiwa kula chakula kilichopikiwa humo. Hivyo, hali ya mwanamke huyu kupikia bafuni ni ya kutatanisha na haifai hata kidogo. Bafuni watu huenda kuoga. Basi iweje chakula kikapikiwa bafuni na kuoga kukatendeka jikoni? Tabia kama hii haikubaliki popote kwa kiumbe razini. Matamshi ya usutaji kama haya hutumiwa na wanawake kuchongoana ili kuonyesha uzuri na ubora wao uliowapelekea kuteuliwa na mwanamume dhidi ya wanawake wenzao. Mengi huwa yamepigiwa chuku ili kumpaka tope mpinzani asipate nafasi yoyote katika maisha ya mwanaume wanayemng'ang'ania.

Katika muktadha ulioigizwa, mwanamke anayejisifu anamkejeli mwenzake kuwa hafai kitu, hapendeki ila anajiuzi kwa wanaume ambao wanaonekana wakiwa wamepanga foleni nje ya chumba kidogo wakiwa wameketi kwenye benchi kila mmoja wao akisubiri zamu yake. Hii ndiyo hali ya mipasho, matusi yanaendelezwa bayana bila aibu. Mwanamke mrejelewa anaonekana akitoka nje na kibatari mkononi akiwaita ndani wanaume waliosubiri mmoja baada ya mwingine ili kushiriki ngono nao. Hatimaye, anakuwa gumzo mtaani ambapo watu wanaonekana wakimsema pale anapopita kutokana na tabia yake mbaya ya usherati. Isitoshe, mwanamke huyu ambaye anarejelewa kama 'mshamba' anaonekana katika kanda hii akipikia bafuni huku akiogea jikoni. Huenda ikawa hii ndiyo sababu ya mwanamume wanayebishania kumkataa na kuwatafuta mwanamke mwingine mwenye ujuzi wa mapishi, kujitunza na kumtunza mume. Pia, huenda ikawa ni hali ya kumharibia sifa mwanamke mtajwa ili apoteze hamu ya kuzozania mpenzi na mwanamke husika.

Aidha, katika wimbo huu, mambo ya uganga na maswala ya kishirikina yameigizwa. Mhusika anamkejeli mwanamke mwenzake kuwa katu hamwezi hata akienda kwa waganga na waganguzi na kuwa atamaliza mizizi bure kwani kumlea mume kwataka ujuzi. Mhusika anadhihirisha ufahamu wa vita vya kimapenzi na mazingira yake ambapo wanaobishania mpenzi huweza kuendana hata kwa waganga kama njia moja ya kumpata mpenzi wanayebishania kama ilivyowekwa wazi na kifungu kifuatacho:

37Utamaliza mizizi, waganga na waganguzi

38Talasimu na hirizi, ongeza na vipodozi`

39Kwake hupati nafasi, mimi ndio yake pumzi

Mhusika amefungamanisha uigizaji huu na uimbaji wa *Modern Taarabu-Mipasho* na kuufanya ujumbe wake uvutie na uwe na uhalisia. Hii ni hali mojawapo ambapo mwingiliano tanzu umedhihirika ukiboresha uwasilishaji wa ujumbe. Mwingiliano tanzu umedhihirika tena kwenye uigizaji katika kiambatisho **-Umejuaje Kama Si Umbea-** ulioimbwa na Mwanaidi Shaaban.

34Milango uliyofunga, gonga misumari gonga, fanya ukuta ujenge pia,

35Weka mtu wa kuchunga, hutania kusonga, sasa Mungu kanifungulia,

36Ulie ukining'ong'a, ati mi wa moja kanga, hali ishanibadilikia,

37Jahazi kutoka Manga, kwangu limetia nanga, neema sasa nailalia.

38Hebu domo lako funga, kwangu mimi hutachonga, jua Mungu, ameshanilipia

Katika uigizaji huu, Mwanaidi Shabaan anaonekana akiwa katika jahazi ambalo limetia nanga. Yeye ndiye abiria pekee katika jahazi hili. Huu ni uigizaji wa safari ya maisha yake. Katika mkondo huu wa maisha, kila mja ana hadithi yake. Kuna wale watu ambao huzaliwa katika utajiri na wala hawaujui umaskini ni nini ila kwa kulisikia neno hilo tu. Hata hivyo, kuna watu ambao maisha yao tangu utotoni huwa ni ya taabu, mashaka na matatizo tele yenye kudhihirishwa na umaskini. Katika muktadha wa kifungu kilichonukuliwa hapo juu, mhusika ni miongoni mwa wale walioishi maisha ya umaskini kwa muda mrefu lakini ghafla wakaamka wakiwa wamefanikiwa. Mhusika anaeleza namna alivyobarikwa naye maulana na kujazwa na neema. Kimsingi, katika wimbo huu mhusika anazungumzia baraka tele alizopata katika maisha yake baada ya kupitia changamoto nyingi hapo awali. Anasifu kuwa ametoka katika lindi la umaskini na sasa ni tajiri kutokana na neema ya Mungu. Ndiyo maana akarejelea kuwa wambea walimsema kuwa yeye ni wa kanga moja kama ilivyo katika mstari ufuatao-

36. Ulie ukining'ong'a, ati mi wa moja kanga, hali ishanibadilikia.

Kanga ni vazi ambalo kwa kawaida katika mazingira ya pwani huvaliwa na wanawake. Mwanamke maskini aghalabu atatambuliwa kwa kuvalia kanga ile ile moja kila siku huku aliye tajiri atabadilisha kanga kwani ana nyingi. Vazi hili la kanga huwa na maua na nakshi tofauti tofauti ambayo hulifanya livutie. Isitoshe, kanga huwa inatumiwa katika mawasiliano kwenye ujumbe ambao huwa umeandikwa kwa kurejelea maswala mbalimbali. Wanawake hujipamba kwa kanga zenye kuvutia katika sherehe mbalimbali za Waswahili. Katika kiambatisho tulichonukuu hapo juu, mhusika amefanikwa kutoka kuwa wa kanga moja na sasa ana kanga nyingi kuashiria kwamba maisha yake yamebadilika na kuwa tajiri. Mungu amemkumbuka mhusika kama alivyodokeza katika ukokotaji ufuatao:

37. Jahazi kutoka Manga, kwangu limetia nanga, neema sasa nailalia.

Kwa kawaida jahazi kutia nanga humaanisha kuwa limefika na safari imefikia hatima yake. Katika maisha ya kawaida, kila mja ana safari yake. Safari hii inaweza huwa na mikondo tofauti katika nyakati tofauti. Mikondo hii wakati mwingine huwa ni ya karaha lakini wakati mwingine ikawa ni

ya baraka. Hii ndiyo maana Waswahili wakasema kuwa 'Hujafa hujaumbika'. Hivyo, katika muktadha huu, jahazi la neema limetia nanga katika maisha ya mhusika huyu na kufanikisha maisha yake. Hii ni baada ya yeye kupitia hali yake ya karaha. Sasa kipindi cha baraka katika maisha yake kimewadia.

Matumizi ya jahazi katika uigizaji huu yanaonyesha kuwa mhusika anayafahamu mazingira yake. Usafiri wa sehemu ile mara nyingi huhusisha vyombo vya kusafiri baharini ambavyo hupitia na kutia nanga katika visiwa mbalimbali vilivyomo. Mhusika anaonekana akiwa ameshika makafi ya kuendeshea mashua, hali inayoashiria kudhibiti usukani wa maisha yake. Maisha yake hayana msukosuko tena, yamekwisha tulia sasa.

Hitimisho

Makala hii imejadili na kufafanua kwa kutolea miktadha ya utanzu wa maigizo kama ilivyojitokeza katika nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho*. Huu ni uigizaji ambao umeingiliana, kusukana na kukamilishana na utanzu wa *Modern Taarabu-Mipasho* katika kuboresha uwasilishaji wa ujumbe. Katika mbinu za utafiti, nilichanganua utanzu huu kwa kukokota maneno, virai, vishazi, sentensi, aya na vifungu vya habari katika muziki teule wa *Modern Taarabu-Mipasho* ili kusesitiza uwepo na umuhimu wa mwingiliano tanzu katika *Modern Taarabu-Mipasho*. Nimerejelea mifano kadhaa kama vile kiambatisho **3MC-Mpenzi Chocolate** ambapo mhusika ambaye ni Mzee Yusuf ameweza kuanza kwa uigizaji akitua kutoka kwa ndege aina ya helikopta. Uigizaji huu unaingiza utanzu wa masimulizi kupitia kwa fomula ya ufunguzi. Hili ni dhihirisho tosha kuwa mwingiliano tanzu kati ya *Modern taarabu-Mipasho* na utanzu wa maigizo katika fasihi simulizi ya Kiswahili ni jambo ambalo hutokea moja kwa moja ama kwa msanii kupanga au kisadfa. Katika uwasilishaji wake, tanzu hizi ziliingiliana na kubadilikabadilika katika uwasilishaji wa utanzu mmoja bila ya kuathiri hadhi ya utanzu huo.

Marejeleo

Bakhtin, M.M. (1981). *The Dialogic Imagination: Four Essays*. Ed. Michael Holquist. Trans. Caryl Emerson and Michael Holquist. Austin and London: University of Texas Press.

Muiruri, P. K. (2006). *Maandalizi Mufti ya K.C.S.E Fasihi Simulizi, Maswali na Majibu*. Palco Enterprises Ltd.

Mulokozi, M. M. (1989). Tanzu za Fasihi Simulizi. Katika, *Mulika. Na. 21*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mpenzi Chocolate-Mzee Yusuf

1. Utangulizi;
2. Imefika siku yenu, nyie kuwaambia kweli,
3. Huo unafiki wenu, na huo ufedhuli,
4. Hatuachani kwa maneno yenu, labda pindijalali,
5. Endeeleni na mirundo,
6. Sie tumependana,
7. Yeye ndio chocolati wangu, na mimi kwake kali,
8. Moyoni adhiti wangu, anayenificha baridi kali,
9. Basi naukweni, nakutamani wewe,
10. Unifiche baridi, mwili joto uwe,
11. Unaponukia udi, malaika hunisimama mie,
12. Hamu hamu hizi, hebu nikumbatie
13. Poleni nyie mafisadi, au wenye roho za ukaidi,
14. Yeye ndio wa uwaridi, raha zake kwangu huzidi,
15. Ananipa raha, ananipa raha ndani ya roho,
16. Nawapa karaha, nawapa karaha munaumwa roho,
17. Meseji zenu zenu zenu za karaha, Mie hazi, hazi nirushi roho,
18. Hamtaki sisi tule raha, tutazidi kuwaumiza roho

19. Kiwe kimoto ananipulizia, nikiwa na joto ananipepea,
20. Mzigo mzito huja kunitua, enye koroto ananifulia
21. Ye ndio kila kitu kwangu, mpenzi chocolate,
22. Ye ndio binti wangu sisikizi yoyote,
23. Kama ni tamu,
24. Nairamba, alivyotia,
25. Kama ni hamu,
26. Naipenda, aniswabilia
27. Ananitia nakshi, nakshi mahamumu,
28. Kumwacha sitaki, nitajidhulumu.
29. Kidonda tamu nzi ndo hufia,
30. Hapa patamu ndio maana nimetulia
31. Dhahari wazimu japari nimevua
32. Ananitia akshi, akshi mahamumu,
33. Kumwacha sitaki, nitajidhulumu.
34. Wanatamani tuachane,
35. wapi, shanshuu, Tuacheni tulale,
36. Na raha tuzile,
37. Ananitia akshi, akshi mahamumu,
38. Kumwacha sitaki, nitajidhulumu.
39. Halua, halua,
40. Halua, halua,
41. Halua, halua,
42. Halua, halua,
43. Halua halua, halua,
44. Halua, halua,
45. Haya ukitaka halua we chukua,
46. Halua, halua,
47. Ukitaka na tende pia chukua,
48. Halua halua
49. Uchungu moyoni unaniwa,
50. Halua halua
51. Halua halua, halua,
52. Halua, halua,
53. Nakuona tu, unanifuatilia,
54. Mi nakuona tu, unaning'ang'ania,
55. Japo sitaki we wanifuatilia,
56. Japo sitaki we waning'ang'ania,
57. Nakuona tu, unanifuatilia,
58. Japo sitaki we waning'ang'ania,
59. Umerogwa wewe mwenzetu, Ulirogwa ama umetumwa,
60. Umerogwa.
61. Nei nei babuji,
62. Chuma chuma dede,
63. Nei babuji,
64. Chuma chuma dede,
65. Chuma, chuma,
66. Chuma chuma dede,
67. Ramaskhe babuji,
68. Chuma chuma dede,
69. Utanibeba leo, umekula hela zangu,
70. We utanibeba leo, umekunywa soda zangu,
71. Utanibeba leo, umekula hela zangu sana,
72. We utanibeba leo, siondoki peke yangu,
73. Utanibeba leo, umekula hela zangu,
74. Maneno maneno, mimi siwezi,
75. Kubishana bishana ovyo siwezi,
76. Kugombana gombana ovyo siwezi,
77. Kubishana bishana ovyo siwezi,
78. Nachokiweza labda ni kazi,
79. Hapo chacha,
80. Mimi ninasema ukweli,
81. Hapo chacha
82. Kimya wewe,
83. Helua, helua,
84. Helua, helua,
85. Helua, helua,
86. Haya ukitaka halua we chukua,
87. Halua, halua,

88. Ukitaka na tende pia chukua,
89. Halua halua
90. Haya ukitaka halua we chukua,
91. Halua, halua,
92. Uchungu moyoni unaniuwa,
93. Halua halua
94. Wanaonipenda wanipende,
95. Wanaonichukia na waende zao,
96. Ala, mpende akupendaye,
97. Asokupenda mtimue,
98. Mpende akupendaye, asokupenda usimng'ang'anie
99. Mpende akupendaye
100. Asokupenda mtimue,
101. Mpende akupendaye, asokupenda achana naye
102. Mpende akupendaye
103. Asokupenda mtimue,
104. Mpende akupendaye, asokupenda usimng'ang'anie
105. Mpende akupendayeasokupenda mtimue,
106. Haraka haraka haraka aende kule,Asije akakuu bure.
107. Halua halua, halua halua,
108. Haya ukitaka halua we chukua,
109. Halua, halua,Ukitaka na tende pia chukua,
110. Halua halua
111. Haya ukitaka halua we chukua,
112. Halua, halua,
113. Uchungu moyoni unaniuwa,
114. Halua halua

Full Stop-Khadija Kopa

Utangulizi;

1. Hamisi Simba, mwana nyamala, waambiana kuja.
2. Wamekataa corner wanakubali penalty.
3. kwa mara nyingine tena,
4. Mimi ni mtu wa watu, nisojua kunong'ona.
5. Jamani mapaparazi, mtajuta kuniona mnaingilia mapenzi,
6. Unayo peana na bwana mlianza na mizizi,
7. Penzi si la mwaka jana, hatukuingia juzijuzi jiji la Dar-es-Salama.
8. Umenipandia ngazi, ukashuka na milima.
9. Umelipiga mapenzi, joto joto lazizima.
10. Atayejitia bazazi
11. Ajue hana usalama.
12. Nitamfungia kazi,
13. Na mji atauhama
14. pamoja salamu klabu.
15. Twendekazi.
16. Fullstop wote kimya, zubaisha king'ori naongea.
17. Fullstop acheni kelele, na si rukhsa kujitetea.
18. Ole wenu mnaopita, njia za panya kunifuatilia.
19. Mimi niko majoha mando wa kike, hala ntawaarifu aaah!
20. Tena nalipa, Bishufi wa ukweli,
21. na nnajua kunengua.Kanipenda, kanizimikia ukweli,
22. nahasa pale, naporembua.
23. Sasa wezi wa mabwana, nawaambia mtawachwa katwaa.
24. Nawapa onyo 'full stop', hii ni challenge full gear.
25. Nyie, taipu zenu za vichochoroni, ndio zinazowafaa.
26. Sio wangu mimi, chumba na varanda tena ghorofani nampandia.
27. Fullstop jipangeni upya, hapa kwangu mumechemka.
28. Nina ladha tamu sana, ndio maana hataki kutoka.
29. Hata mje na waganga lori nzima, himaya yangu keshafika.
30. Mnilie mizimu na makafara, na mchinje hata paka.
31. 'Full stop' jipangeni upya, hapa kwangu mmechemka.
32. Nina ladha sweeti sana, ndio maana hataki kutoka.
33. Hata mje na waganga lori nzima, himaya yangu keshafika.
34. Mnilie mizimu na makafara, na mchinje hata paka.
35. Halafu wajifanya unalipa, hutafuti wako ukamweka.
36. Wewe huezi miliki yangu, baby cute wa Kiafrika.
37. Kwanza mimi niko peke yangu, nimetulia sina shaka.
38. Nimetulia na mume wangu, mtoto wa uhakika.
39. Vikarolaiti vyenu, vinavyowapa jeuri,

40. Hivyo vikarolaiti vyenu, nitavipiga marufuku hapa.
41. Mimi nina rangi yangu, sitaki uso wa baka.
42. Mimi nina rangi yangu, na tena bado nawaka.
43. Bandika bandika, mimi nabandua.
44. Nikuhidi maarifa, huna unalolijua.
45. Bandika bandika, mimi nabandua.
46. Tumependana wawili, wewe unajijua.
47. Hakutaki pesa mbili, hulijui takataka.
48. Bandikabandika, mimininabandua.
49. Bandikabandika, mimininabandua.
50. Semasema, Musa Musa. Musa mipango.
51. Mfalme wabesi Tanzania.
52. Wametoka kwa Harita .
53. Tumependa na wenyewe, maneno maneno ya nini.
54. Eti Zera naughty boy, kwani mnataka nini?
55. Sasa ninawaambia kijana yuko makini.
56. Wala hahitaji foja, maximum nikochini.
57. Hahitaji msichana wa jezi, kiwanda anachondani.
58. Anavyotua vifaa, kama yuko Marekani.
59. Kama yuko Marekani.
60. Usigusemoto utapunguza.
61. Napajua hapa Bongo, pameeneavituko.
62. Nakujua kule Zeni, kumeeneavituko.
63. Na Mombasa mjini, pameeneavituko.
64. Kina dada wakwambia, mambo nimpambaiko.
65. Kama hujajipodoa, hapa Bongo hunasoko.
66. Hapa Bongo huna soko.
67. nikwelezeje hunasoko.
68. Ninakuwekakipupa, nakupasahunasoko.
69. Usigusemoto utapunguza, usigusemotoutapunguza.
70. Na kina dada wa bongo, wakweli wajanjasana
71. Kina dada wa Mombasa, nanyiewajanjasana,
72. Na kina dada wa Zenji, kwakweli wajanjasana,
73. Mkifikauwanjani, macho mnatazama.
74. Sasamkitokanje, mnawagobeamabwana.
75. Mnagobeamabwana, mnagobeamabwana.
76. Eeeh usiguse moto, utakuuguza,
77. Eeeh usiguse moto utakuguza.
78. Wapenzi wangu nawapenda, usifikiriutani,
79. I love you so much, usifikiriutani.
80. Nimewamiss, usifikiriutani.
81. Wapenzi wangunawapenda, usifikiri utani.
82. Hatamnapochizika, naposimama stejini,
83. Na pale mnapopagawa, napokuwa uwanjani,
84. Mungekuwa embe dodo, ningewala na majani.
85. Ningewala na majani, ningewala na majani.
86. Usigusemoto, utapunguza, usigusemotoutapunguza.
87. Watotowanguwakiume, nisikilizeninyie,
88. Mnaojiitamasharobaro, nisikilizeni.
89. Nyiemabarobaro, nisikilizeni.
90. Nawaambia kina kaka, wanawakewanajua.
91. Pale pana pa utamu, wamepapambamaua,
92. Ukikosa gonorrhea, ukimwiutakuuwa.
93. Ukimwiutakuuwa, ukimwiutakuuwa.
94. Usigusemoto, utapunguza,
95. Usigusemoto, utapunguza.
96. Kimalizio;
97. Totimoto, watuache.
98. Totimoto, tupishetupite.
99. Totimpangomzima,
100. Totimpangomzima.
101. Loliondo kwa babu, sharubaru kapewa kikombe

Akasema nangoja mrija boi.

Utalijua Ijji-Afua Suleiman

Utangulizi;

1. Kazi yako ufasidi Jeuri ngebe na nongwa
2. Baraka ya ukaidi Ukali kama embe ngwangwa
3. Vituko vya makusudi Si bure we umerogwa

4. **Badala ya soda baridi Ama juice ya chungwa**
5. **Ushamba umekuzidi Andazi wanywia togwa**
6. **Mwenzangu huna ujuzi Mpenzi umemuudhi**
7. **Kaja kwangu nimempokea.**
8. Pokea chako kibomu Shoga nakutumia
9. Hata ukinilaumu Wako nishamchukua
10. Penzi ulimdhulumu Visa ukamfanyia
11. Chachandu vitamtamu Bwana hukumpatia
12. Bwana kapata wazimu Kashindwa kuvumilia
13. wangu akatia timu Tiba nikampatia
14. Nikampa vitu adimu Kwako hajajionea
15. Amri akasalimu Magoti kunipigia
16. Huku akijilaumu Kwako kapotea njia
17. Kapenda yangu nidhamu Na utulivu nyumbani
18. Pamoja na ukarimu Kwa ndugu na majirani
19. Ucheshi na tabasamu Kanijalia manani
20. Nimepewa lugha tamu Nyoka hutoka pangoni
21. Sifa hizi ni muhimu Na mengi mengine ndani
22. Wewe mkaanga sumu Kwako hazipatikani
23. Na mapishi yako bomu Kitimutimu jikoni
24. Wali wautia ndimu Hayo ni mapishi gani
25. Bwana imemwisha hamu Katimua nyumbani
26. Unaningoja njiani Madhila kunifanyia
27. Usitake ushindani Hunishindi nakwambia
28. Mimi naletewa ndani Wewe watanga na njia
29. Magomeni BuguruniNdala za kukatikia
30. Wasela wa vijiwaniNafuu wajipatia
31. Uroda kwa foleni Kwako wajipendelea
32. Wewe gumzo mjini Watu wanahadithia
33. Umeachika ndoa niniKwa yako mbaya tabia
34. Unaogea jikoni Bafuni unapikia
35. Kwako kaachia ngazi Kwangu kaweka makazi
36. Sasa akaa mbalizi Kachoka yako maudhi
37. Utamaliza mizizi Waganga na waganguzi
38. Talasimu na hirizi Ongeza na vipodozi
39. Kwake hupati nafasi Mimi ndio yake pumzi
40. **Sasa ndo utalijua jiji mwenzangu**
41. **Chajio utakunywa uji mwenzangu**
42. **Na juice utakunywa maji mwenzangu**
43. **Huyu kwako harudi tena mwenzangu**
44. **Najinafasi najinafasi**
45. **Utajiju wewe utajiju**
46. Kwako nishamchukua Kwako harudi tena we mwenzangu
47. **ohh utalia mwenzangu jiji utalijua**
48. Katamka waziwazi Kuwa hakutaki tena we mwenzangu
49. **ohh utalia mwenzangu jiji utalijua**
50. Bwana kanipa nafasi Nimuonyeshe ujuzi we mwenzangu
51. **ohh utalia mwenzangu jiji utalijua**
52. Nami sifanyi ajizi Mpenzi namuenzi we mwenzangu
53. **ohh utalia mwenzangu jiji utalijua**
54. Nampikia maandazi Na chai ya tangawizi we mwenzangu
55. **ohh utalia mwenzangu jiji utalijua**
56. Wali wa nazi kwa ndizi Mavitus kama kazi mwenzangu we mwenzangu
57. **ohh utalia mwenzangu jiji utalijua**
58. Mwisho natoa dozi Impayo usingizi we mwenzangu
59. **ohh utalia mwenzangu jiji utalijua**
60. Mwenzangu huna ujuzi Rudi tena kajifunze we mwenzangu
61. **ohh utalia mwenzangu jiji utalijua**
62. Bibi acha upuuzi Kuishi na mume kazi we mwenzangu
63. **ohh utalia mwenzangu jiji utalijua**
64. Mume ataka malezi Sio mambo ya kihuni we mwenzangu
65. **ohh utalia mwenzangu jiji utalijua**
66. Ngebe na jeuri zako Leo zimekuishia we mwenzangu
67. **ohh utalia mwenzangu jiji utalijua**
68. ohh utalia mwenzangu jiji utalijua wee

Umejuaje Kama Si Umbea- Mwanaidi Shaaban

1. Utangulizi;

2. Umejuaje*3
3. Umejuaje nimefanikiwa umejuaje?
4. Umejuaje ukaonafi umejuaje?
5. Umejuaje kama si umbea umejuaje?
6. Umeyatafuta, umeshayapata, sasa walialia
7. Vizurivyakupita, wavikodolea macho,
8. Vinono vyakupita wavikodolea macho
9. Vitamu vyakupita wavikodolea macho
10. Wakufuma tumefuma, fuma,wakukosa umekosa, kosa
11. Swadakta, umepata swadakta,
12. Swadakta, nimefanikiwa swadakta,
13. Umesikika waamba, wewe bado unagomba, lipi likusumbualo jambo?
14. Macho yako kama mamba, wala hujui kufumba, hakikupiti kitu kirembo,
15. Japo mie sijatamba,wala sio wa kujigamba,lakini sifichi langu pambo,
16. Kasirika sasa vimba, bure jua hutaziba, wewe jifunze ujue mambo.
17. Endelea kunichimba, nenda kwa wachawi omba, jua Mungu hapigi kwa fimbo,
18. Adabu yako elewa, nimefanikiwa mie,
19. Kiitikio;
20. Jahaza yako elewa nimefanikiwa mie
21. Nimeongokewa mie,
22. Nimejaliwa mie,
23. Unaona fi,kuniona mie kung'aa,
24. Siachi*4, kuvaa mie siachi.
25. Unaona fi,mie kupanda Rav.4 ,
26. Siachi*4, kupanda Rav4 siachi.
27. Unaona fihi,mie kuenda melody ,
28. Siachi, kuenda melody siachi.
29. Wataka kuliziba jua na ungo,
30. Huwezi kuliziba jua,
31. huwezi kuliziba na ungo,
32. Huwezi kuliziba jua,
33. Huwezi kuliziba.
34. Milango uliyofunga, gonga misumari gonga, fanya ukuta ujenge pia,
35. Weka mtu wa kuchunga, hutaniona kusonga, sasa Mungu kanifungulia,
36. Ulie ukining'ong'a, ati mi wa moja kanga, hali ishanibadilikia,
37. Jahazi kutoka Manga, kwangu limetia nanga, neema sasa nailalia.
38. Hebu domo lako funga, kwangu mimi hutachonga, jua Mungu, ameshanilipia
39. Kiitikio;
- 40. Jaza yako elewa, nimefanikiwa mie,**
- 41. Nimeongokewa mie, nimejaliwa mie.**
- 42. Unaona fi, uliona mie kung'aa,**
- 43. Siachi, kung' aa mie siachi.**
- 44. Unaona fi,mie kupanda Rav4 ,**
- 45. Siachi, kupanda Rav4 siachi.**
- 46. Unaona fi,mie kuenda melody ,**
- 47. Siachi, kuenda melody siachi.**
- 48. Wataka kuliziba jua na umbo,**
- 49. Huwezi kuliba jua, huwezi kuliziba na umbo,**
- 50. Huwezi kuliziba jua, huwezi kuliziba.**
- 51. Kimalizio;**
52. Kalichagua goma, la Kiswahili goma,
53. Chakacha namchezea, habibi namchezea
54. Lele mama namchezea, habibi namchezea
55. Msewe namchezea, habibi namchezea,
56. Hatakiririani yako, kalichagua bada langu.
57. Sima ya bada hujui kusonga, hujui kusonga sima ya bada.
58. Sima ya bada tamu,
59. ipate mpishi timamu.
60. Ipate papa adhimu,
61. Utie na tui gumu,
62. Pia chachandu ya ndimu
63. Ukilahuishi hamu, huishi hamu kuila.